

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TISA

KIKAO CHA TISA

10 NOVEMBA, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TISA

KIKAO CHA TISA – TAREHE 10 NOVEMBA, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

127. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaongezea mkopo Akinamama Wajasiriamali wa Mkoa wa Katavi.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

128. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, ni lini Serikali itaajiri Wahitimu wa Kada ya Mazingira waliomaliza katika Vyuo Vikuu nchini.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

129. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, nini kauli ya Serikali kwa Wakulima wa Vitunguu maji katika Bonde la Eyasi juu ya upatikanaji wa masoko pamoja na bei ya zao hilo.

130. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha TBS na ZBS zinafanya kazi kwa ushirikiano.

WIZARA YA MAJI:

131. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya mradi wa maji wa Kiwira ili uanze kutekelezwa.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

132. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Kituo cha Polisi Tarafa ya Kintinku Manyoni.

133. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Vituo vya Polisi katika Tarafa za Gonja na Mamba/Vunta.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

134. MHESHIMIWA FRANCIS ISACK MTINGA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya katika Halmashauri ya Mkalama.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**135. MHESHIMIWA KASALALI EMMANUEL
MAGENI (SUMVE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya Fulo kupitia Nyambiti hadi Malya itafanyiwa upembuzi yakinifu na kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

**136. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA
(LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa barabara ya Mnivata – Masasi kupitia Tandahimba na Newala.

WIZARA YA AFYA:

**137. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI
KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imejipangaje katika kupambana na changamoto ya upungufu wa Wataalam wa Mazoezi Tiba na huduma ya Utengamao nchini.

138. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna utafiti wowote ambao umefanyika ili kubaini dawa za ganzi/nusu kaputi zinazosababisha vifo kwa wanaojifungua kwa upasuaji.

III. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka 2023/2024 pamoja na Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
10 NOVEMBA, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**